JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

**Dar es Salaam, 07 Agosti 2026.**

## TAARIFA KWA UMMA

## USIMAMISHWAJI WA MUDA WA UAGIZAJI NA UUZWAJI WA BIDHAA ZA POMBE NCHINI RWANDA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kutaarifu wafanyabiashara na umma kwa ujumla kuwa limeona tangazo lililotolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Rwanda (Rwanda FDA) la tarehe 05 Agosti, 2026 kuhusu kusimamishwa kwa muda uagizaji na uuzwaji wa baadhi ya bidhaa za pombe nchini humo kutoka nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

TBS inapenda kuwahakikishia wafanyabiashara na umma kwamba bidhaa zote za pombe zilizoorodheshwa katika tangazo hilo ambazo zinazalishwa nchini Tanzania, zimethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufuatia kukidhi vigezo vya ubora kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki ya Viwango, Udhibiti Ubora, Metrolojia na Upimaji (EAC SQMT Act 2006).

Aidha, Shirika kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara linafuatilia suala hilo katika ngazi mbalimbali, ikiwemo Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi husika ili kupata suluhu ya suala hilo mapema iwezekanavyo.

Shirika linatoa wito kwa wafanyabiashara wa bidhaa husika na umma kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho mawasiliano yanaendelea.

Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800 11 0827,** ofisi ya TBS iliyo karibu nao au ofisi ya Halmashauri.

**Imetolewa na:**

Digitally Signed By Gladness H. Kaseka
Fri Aug 07 19:44:27 EAT 2026

Gladness H. Kaseka

**Meneja Uhusiano na Masoko**

***"Kuchochea Ubora na Usalama kwa Maisha Bora"***


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma /
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo:
0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**KANDA YA ZIWA-MAGHARIBI**
S.L.P 816,
OFISI YA MKUU WA MKOA - Ghorofa ya Tatu
GEITA

**TBS KANDA YA ZIWA MASHARIKI**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA MASHARIKI**
Jengo La Manispaa KIBAHA
Ghorofa ya Kwanza
KIBAHA, PWANI

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA MAALUM YA DAR ES SALAAM**
Jengo la PSSSF
Ghorofa ya Nne
DAR ES SALAAM,
TANZANIA

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la SOKOINE
S. L. P. 1396
MTWARA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023